

Jina

Nambari Yako

Shule

Sahihi

Tarehe

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

(FASIHI)

JULAI / AGOSTI 2010

MUDA: SAA 2 ½

MTIHANI WA PAMOJA – WILAYA YA LAIKIPIA 2010

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Upile

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

(FASIHI)

MUDA: SAA 2 ½

MAAGIZO:

- Jibu maswali manne pekee. Swali la kwanza ni la lazima.
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki : Tamthilia, Riwaya, Ushairi na Fasihi Simulizi

Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa, watahiniwa lazima wahakikishe kurasa zote zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo.

MAYAI WAZIRI WA MARADHI NA HADITHI NYINGINE

A 1. SWALI LA LAZIMA

Mayai Waziri Wa Maradhi Na Hadithi Nyingine – K W Wamitila

Kwa kurejelea hadithi ya UTEUZI WA MOYONI na NGOME YA NAFSI, thibitisha ukweli kwamba mwanamke amedhalilishwa sana katika jamii zetu. (alama20)

B RIWAYA

Utengano – Said A. Mohamed

2. Fafanua nafasi ya mwanamke kama ilivyosawiriwa na mwandishi wa Riwaya ya Utengano. (alama20)
3. Utengano ni anwani mwafaka kwa Riwaya hii ya S. A. Mohamed. Eleza ukweli wa kauli hii, kwa kutoa mifano yoyote mitano. (alama20)

C TAMTHILIA

Kifo Kisimani – Kithaka wa Mberia

4. Huku ukitolea mifano ifaayo, onyesha mbinu alizotumia Mtemi Bokono kuitawala Nchi ya Butangi. (alama20)

D USHAIRI

5. Linganisha na kutofautisha mashairi ya ARUDHI na MASHAIRI HURU (alama20)
6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

- | | | |
|---|--|---|
| 1. Hisani inanyanyuza,
Mdogo ikamkuza,
Kinda ikamtukuza
Hisani ikamlea. | 6. Ihsani haiozi,
Mfano kama mizizi,
Zaidi ya utoshezi,
Unapoitumilia. | 9. Nanyi ndugu fikirini,
Muikumbuke hisani,
Hαιοzi ihisani,
Daima huchipukia |
| 2. Hisani na ukarimu,
Hadi ni vitu muhimu,
Mfanowe mlizamu,
Hisani kufadhiliwa. | 7. Hisani ni kama fimbo, 12.
Husotea hata ng'ambo,
Ikawavuta warembo
Hisani bila udhia. | Hisani yanipa sifa,
Yanongeza maarifa,
Na hata kama nikifa
Wanangu watatumia. |
| 3. Hisani kama Johari,
Haipati mjasiri,
Ni Joho lenye fahari,
Hisani ukitumia | 8. Hisani njema huweka, 13.
Ni akibayo ya myaka,
Japo wito kiitika,
Hisani itasalia. | Watatumia maisha,
Hisani nilobakisha,
Hadi mwisho wa maisha
Na kuondoka dunia, |
| 4. Basi sikia watoto,
Hisani ni jambo zito,
Si pesi kama kokoto,
Si kitu cha kubeua. | 9. Ikupe mema makazi, 14.
Wewe na wako uzazi,
Iwe kama sumlizi,
Na wana wakitumia. | Najua mtakubali,
Haya bila ya shikeli,
Asiyejua fadhili,
Nyama kasoro mkia. |
| 5. Hisani yaweza kupa,
Utajiri kukukopa,
Ukaweza kunenepa,
Lafidhi njema kutoa, | 10. Basi dunia si fosi,
Yataka mwendo wa ngisi,
Wawapi kina Msosi,
Nguvu walikitumia. | |

- a) Fafanua arudhi zilizotumiwa kutunga shairi hili (alama4)
- b) Kina kinachokaririwa sana katika shairi hili huitwaje? (alama1)
- c) Shairi hili huitwaje? (alama1)
- d) Ukirejelea shairi hili, fafanua sifa za mashairi ya aina hii (alama4)
- e) Ni upi ujumbe wa mshairi? Toa mifano minne (alama4)
- f) Taja na ufafanue mifano minne ya mbinu za matumizi ya lugha katika shairi (alama4)

- g) i) Linganisha na kutofautisha maneno
'Hisani na lhisani' (alama1)
- h) Taja mstari unaolingana kimaana na
'Japo wito kiitika' (alama1)

E

FASIHI SIMULIZI

7. a) Methali ni nini? (alama2)
- b) Ainisha sifa Tano za methali za Kiswahili (alama10)
- c) Elezea umuhimu wa hadithi kama utanzu wa fasihi simulizi
katika jamii (alama8)